JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

BARAZA LA SANAA LA TAIFA - BASATA

# MWONGOZO WA UENDESHAJI WA MASHINDANO YA UCHORAJI 2025

Umeidhinishwa na Baraza Tarehe 17 Novemba, 2025



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

**BARAZA LA SANAA LA TAIFA- BASATA**

# MWONGOZO WA UENDESHAJI WA MASHINDANO YA UCHORAJI

**Umeidhinishwa na Baraza Tarehe 17 Novemba, 20205**

**Umetolewa Na:**

Katibu Mtendaji - BASATA

S. L. P. 4779

**Dar es Salaam.**

## YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| 1. | UTANGULIZI ………………………………………………………………… | 2 |
| 2. | CHIMBUKO ………………………………………………………………… | 2 |
| 3. | MADHUMUNI ………………………………………………………………… | 3 |
| 4. | MAZINGATIO YA JUMLA NA MAHUSUSI …………………………… | 3 |
| | 4.3.1 Haki na usawa ……………………………………………………… | 4 |
| | 4.3.2 Taarifa sahihi ……………………………………………………… | 5 |
| | 4.3.3 Uadilifu ……………………………………………………………… | 5 |
| | 4.3.4Ubora wa shindano ………………………………………………… | 5 |
| | 4.3.5 Ufanisi wa waandaaji ……………………………………………… | 5 |
| | 4.3.6 Wajibu wa kisheria ………………………………………………… | 6 |
| | 4.3.7 Maadili ……………………………………………………………… | 6 |
| | 4.3.8 Majaji ………………………………………………………………… | 6 |
| | 4.3.9 Haki za Watoto …………………………………………………… | 7 |
| | 4.3.10 Watu wenye Mahitaji Maalum ……………………………….. | 7 |
| | 4.3.11 Huduma za afya …………………………………………………… | 7 |
| | 4.3.12 Mialiko kwa wageni rasmi ………………………………………… | 7 |
| 5. | WAHUSIKA WA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO ………………… | 8 |
| 6. | MAMLAKA YA BASATA YA KUSIMAMIA MASHINDANO …………… | 8 |
| 7. | MAREKEBISHO ……………………………………………………………… | 9 |
| 8. | MAKOSA NA ADHABU ……………………………………………………… | 9 |
| 9. | TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA …………………………………… | 9 |
| 10. | VIAMBATISHO ……………………………………………………………… | 10 |

**Tafsiri ya Maneno**

**BASATA** – maana yake ni Baraza la Sanaa la Taifa;

**kibali –** ruhusa inayotolewa na BASATA kwa mwendeshaji wa shindano la uchoraji;

**kumbi** – maana yake ni jengo ama eneo lolote linalotumika kwa ajili ya kazi za Sanaa, sherehe au burudani;

**maadili** - litajumuisha tabia njema, misingi, kanuni, au taratibu zinazofuata mienendo inayokubalika katika jamii, ambayo inaongoza uhusiano katika makundi ya jamii inayohusika isiyovunja mila na desturi za Mtanzania;

**mdau wa Sanaa** – ni mtu yeyote, taasisi au kampuni inayojishughulisha na masuala ya sekta ya Sanaa moja kwa moja au vinginevyo;

**msanii** – mtu yeyote anayefanya kazi ya Sanaa kwa mujibu wa Sheria inayohusu masuala ya Sanaa nchini.

**mwongozo** - ni Mwongozo wa Uendeshaji wa Mashindano ya Uchoraji;

**sanaa za ufundi**- litajumuisha uchoraji, uchongaji, ususi, utanashati na ulimbwende, ubunifu wa mavazi;

**sheria** - maana yake ni Sheria ya BASATA, Sura ya 204 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019;

**shindano** – litajumuisha mashindano ya Sanaa na burudani pamoja na mashindano yasiyo ya Sanaa ambayo yanatumia wasanii;

**uchoraji** – sanaa ya kuweka alama au picha kwa kutumia vifaa mbalimbali vya kuchorea kama vile, kalamu ya wino au risasi, bulashi, penseli za rangi na vifaa vingine.

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya BASATA ya Mwaka 1984, Sura ya 204 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019. Kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya BASATA majukumu ya BASATA yanajumuisha kufufua, kukuza na kuendeleza sekta ya Sanaa, kuratibu na kutoa vibali kwa mashindano yote ya Sanaa yanayofanyika nchini.

1.2 Katika zama za hivi karibuni Sanaa imekuwa kazi na ajira, hivyo kusababisha idadi kubwa ya wasanii na kazi za Sanaa kuongezeka kwa kasi sanjari na ukuaji wa teknolojia. Hii imeambatana na kuongezeka kwa mashindano ya Sanaa hapa nchini ambapo pamoja na majukumu mengine BASATA ina jukumu la kuratibu, kutoa vibali na kusimamia Mashindano ya Uchoraji.

1.3 Ni dhahiri kuwa kwa sasa Sekta ya Sanaa imekua, hivyo usimamizi unaofaa ni ule unaoweka mazingira yanayoijenga Sekta kuwa rasmi na kazi za Sanaa kuwa njia ya kuinua uchumi badala ya burudani pekee. Hata hivyo, ni lazima kuzingatia Kanuni za uandaaji na uendeshaji wa Mashindano ya Uchoraji.

1.4 Mwongozo huu ni maelekezo kwa wasanii, wadau wa sanaa, taasisi, vikundi na mtu yeyote anayejighulisha na sanaa.

## 2.0 CHIMBUKO

2.1 Uchoraji umekuwa unafanyika kwenye jamii za Kitanzania kwa muda mrefu kwa lengo la kuburudisha, kuelimisha, kuwasiliana na kuweka kumbukumbu za historia, tamaduni, maisha na shughuli za kijamii. Awali kumekuwa na mashindano ya jadi ya uchoraji kuhusu ubunifu na ujuzi wa wasanii wa jadi. Katika mashindano hayo, wasanii walitumia mbinu na vifaa vya jadi kuunda kazi za sanaa zinazoonesha utamaduni na mila zao. Kwa sasa uchoraji umekuwa sehemu ya ajira, biashara na chanzo cha mapato tofauti na ilivyokuwa zamani.

2.2 Mwongozo huu ni utekelezaji wa Kanuni za BASATA za Mwaka 2018 zinazoelekeza uzingatiaji wa kanuni katika uandaaji wa mashindano ya Sanaa. Vilevile, Mwongozo huu ni utekelezaji wa Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997 na Mwongozo wa Maadili katika Kazi za Sanaa wa Mwaka 2023.

## 3.0 MADHUMUNI

3.1 Madhumuni ya mwongozo huu ni pamoja na: -

a) Kuwawezesha wasanii na wadau wa Sanaa kwa kuwapa elimu na miongozo ya kuzingatia katika uendeshaji wa mashindano ya uchoraji;
b) Kulinda jamii dhidi ya vitendo vilivyo kinyume na maadili ya Mtanzania katika mashindano ya uchoraji nchini;
c) Kutambua na kuhifadhi utamaduni, ujuzi, mila na ubunifu;
d) Kuendelea kuipa hadhi na thamani tasnia ya Uchoraji;
e) Ni utekelezaji wa Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997 kuhusu kuweka mfumo na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa Utamaduni.

## 4.0 MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA UENDESHAJI WA MASHINDANO YA UCHORAJI

4.1 Kabla na wakati wa shindano, mwandaaji atapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

a) Awe na kibali hai cha kuendesha shughuli za Sanaa kwa mujibu wa Sheria na kanuni za BASATA;

b) Awe amewasilisha maombi pamoja na mchanganuo wa andiko la mtiririko wa shindano husika kupitia Mfumo wa Wadau wa Sanaa (AMIS) siku 30 kabla ya shindano;

c) Shindano lilenge kuelimisha, kuburudisha na kuhamasisha umma katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na kudumisha utamaduni wa Mtanzania;

d) Wasanii watakaoshiriki katika shindano ni sharti wawe wamesajiliwa na kuwa na vibali hai vya BASATA na orodha yao ni sharti iambatanishwe wakati wa kuwasilisha andiko;

e) Shindano litaendeshwa kwa kuzingatia pamoja na mambo mengine, Mwongozo wa Uzingatiaji Maadili katika Kazi za Sanaa, vigezo, mikataba na vipengele vya shindano husika;

f) Ukumbi utakaotumika kwa shindano ni lazima uwe umesajiliwa na kuwa na kibali hai cha kufanya shindano;

g) Isipokuwa kwa kibali maalum, watoto chini ya umri wa miaka 18 hawataruhusiwa kuingia katika ukumbi au sehemu kunakouzwa vileo wakati wa shindano;

h) Isipokuwa kwa kibali maalum, watoto wasiruhusiwe kuwepo katika ukumbi au eneo la shindano baada ya saa 12:00 Jioni;

i) Kwa shindano lenye zawadi zitakazokabidhiwa ziwasilishwe BASATA ndani ya siku 14 kwa ajili ya upekuzi kabla ya shindano;

j) Gharama za usimamizi wa shindano kama zitakuwepo, zitabebwa na mwandaaji wa shindano husika;

k) Mwandaaji atawasilisha vielelezo vinavyodhihirisha uwezo wa rasilimali fedha kuendesha shindano husika;

l) Mwandaaji ataweka mikakati kuhusu utunzaji wa mazingira kwa wasanii na wadau wa sanaa wakati wote wa kuendesha shindano;

m) Kwa mwandaaji atakayetaka kushirikiana na BASATA katika uratibu wa shindano lake atapaswa kuwasilisha maombi rasmi siku 30 kabla ya shindano hilo akionesha maeneo mahususi ya ushirikiano.

4.2 Baada ya shindano, mwandaaji atazingatia mambo yafuatayo: -

a) Kuwasilisha taarifa ya shindano ikiwa katika maandishi na picha zilizohaririwa si zaidi ya siku 14 baada ya shindano kukamilika;

b) Kufanya tathmini ya shindano litakaloshirikisha wadau mbalimbali wa Sanaa husika ndani ya siku 14 baada ya kupokelewa kwa taarifa.

4.3 Pamoja na mambo ya kuzingatia yaliyotajwa, mwandaaji wa shindano atatakiwa kuzingatia vipengele mahususi vifuatavyo katika uendeshaji wa shindano: -

**4.3.1 Haki na usawa kwa washiriki**

4.3.1.1 Waendeshaji wa mashindano watahakikisha kuwa panakuwa na haki na usawa kwa washiriki kwa kuhakikisha kuwa mashindano yanaeleza wazi mambo yafuatayo: -

a) Vigezo vya kupata ushindi;
b) Kutaja ukubwa wa kazi zinazohitajika;
c) Ratiba ikijumuisha Muda wa kuwasilisha kazi;
d) Mahali shindano linapofanyika, kama shindano linahitaji mahudhurio ya washiriki;
e) Vigezo vya shindano, kama vile umri;
f) Utaratibu wa kupata washindi;
g) Matumizi au zuio la matumizi ya akili unde;
h) Kuweka wazi zawadi zinazoahidiwa kwa washindi.

### 4.3.2 Taarifa sahihi na zilizo wazi

4.3.2.1 Waandaaji watatakiwa kutoa taarifa sahihi na zilizo wazi zikiwemo:

a) Mada ya shindano;
b) Aina ya rangi na malighafi zitakazotumika;
c) Mfumo kwa kazi za kidigitali;
d) Mipaka, wigo na nyenzo zinazoruhusiwa;
e) Utaratibu wa kuwasilisha kazi;
f) Uwanda wa matumizi ya vifaa vya kufanyia kazi kama kompyuta.

### 4.3.3 Uadilifu katika shindano

4.3.3.1 Waandaaji wanatakiwa kuzuia:

a) Matumizi ya Kazi za Sanaa zisizo na ruhusa au kibali cha Msanii/Mtunzi halisi;
b) Kunakili au kutumia kazi za mtu mwingine;
c) Mbinu za udanganyifu wakati wa shindano.

### 4.3.4 Ubora wa shindano

4.3.4.1 Waendeshaji watahakikisha kuna ushindani ulio na ubora katika Shindano kwa-

a) Kuwataarifu washiriki juu ya matokeo ya ushiriki wao;
b) Kuhimiza ushindani usiojenga chuki au uadui;
c) Kutambua na kuthamini juhudi zilizofanywa na washiriki.

### 4.3.5 Ufanisi wa waendeshaji

4.3.5.1 Waendeshaji watapaswa:

a) Kuwa na mfumo mzuri wa kupokea na kuchakata kazi za wasanii;
b) Kushirikisha wataalamu husika katika kuchagua majaji wa Shindano;
c) Kuhakikisha kuwa suala la mgongano wa maslahi linadhibitiwa;
d) Kuhakikisha kuwa vigezo vya ushiriki, uwasilishaji kazi na Sheria nyingine za Shindano vinafuatwa;
e) Kutambulisha uwepo au kutokuwepo kwa wadhamini.

### 4.3.6 Wajibu kisheria

4.3.6.1 Waendeshaji wa mashindano watapaswa:

a) Kuheshimu Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki;

b) Kuweka bayana haki ya waendeshaji kutumia, kuonesha au kuchapisha kazi za washiriki;
c) Kuweka bayana mikataba au makubaliano na washiriki;
d) Kuhakikisha kunakuwepo mazingira mazuri ya kuhifadhi kazi za washiriki wakati wa shindano ili zisiharibike;
e) Kutunza taarifa binafsi za washiriki.

#### 4.3.7 Maadili

4.3.7.1 Waendeshaji watahakikisha shindano linazingatia -

a) Kuheshimu na kusimamia maadili ya kitanzania;
b) Kuzingatia Mwongozo wa Uzingatiaji Maadili katika Kazi za Sanaa.

#### 4.3.8 Nafasi ya majaji katika shindano

4.3.8.1 Majaji katika shindano watapaswa -

a) Kuwa na weledi wa fani husika na kuthibitishwa na mamlaka inayosimamia shughuli za Sanaa nchini;
b) Kutoa taarifa mapema juu ya mazingira ya mgongano wa maslahi;
c) Kumruhusu mwenyekiti wa jopo la majaji kupiga kura kumpata mshindi endapo kura za majaji ztalingana;
d) Kuwa waadilifu; wasioshiriki vitendo vya rushwa na wasiotoa siri za uamuzi kabla, wakati na baada ya shindano.

#### 4.3.9 Haki za watoto katika mashindano

4.3.9.1 Endapo mashindano yatahusisha ushiriki wa watoto wasanii, waendeshaji watatakiwa kupata idhini ya shule, wazazi au walezi.

#### 4.3.10 Watu wenye mahitaji maalum

4.3.10.1 Endapo shindano litahusisha watu wenye mahitaji maalum, waendeshaji watatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo: -

a) Waendeshaji waweke miundombinu rafiki kwa washiriki husika;
b) Shindano lisiwe na maudhui yenye kulenga kuwabagua au kuwadhalilisha kwa namna yoyote.

#### 4.3.11 Huduma za afya

4.3.11.1 Mwendeshaji atahakikisha kunakuwepo huduma ya kwanza katika shindano.

#### 4.3.12 Mwaliko kwa Mgeni Rasmi

4.3.12.1 Mwendeshaji wa shindano mapema iwezekanavyo, atawasilisha BASATA maombi ya kumualika Mgeni Rasmi ili kuwezesha kufanyika kwa taratibu nyingine.

## 5.0 WAHUSIKA WA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO

Mwongozo huu utatekelezwa na wasanii, wadau wa sanaa, taasisi, vikundi na watu wengine wowote watakaojishughulisha na sanaa.

## 6.0 MAMLAKA YA BASATA KATIKA KUSIMAMIA UENDESHAJI WA MATUKIO YA SANAA

BASATA itaweka utaratibu mzuri wa uendeshaji wa matukio ya Sanaa hapa nchini na kutoa elimu kuhusu uendeshaji wa matukio.

## 7.0 MAKOSA NA ADHABU

Bila kuathiri kipengele chochote cha Mwongozo huu, mtu yeyote atakayekiuka kipengele chochote katika Mwongozo huu atakuwa ametenda kosa na atachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa.

## 8.0 MAREKEBISHO

Mwongozo huu unaweza kufanyiwa marekebisho endapo italazimika kufanya hivyo.

## 9.0 TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA

Mwongozo huu utaanza kutumika baada ya kupata idhini ya Baraza.

**MWONGOZO HUU** umeidhinishwa na Baraza Tarehe **17 Mwezi Novemba, 2025.**

**KIAMBATISHO 01**

## VIGEZO VYA KUZINGATIA KUMPATA MSHINDI

### 1. Uasili na ubunifu

Katika mashindano ya sanaa, ubunifu na uasilia hufafanuliwa kama ifuatavyo:

### A.Uasilia

i. Kazi ya sanaa inatakiwa kuwa ni ya kipekee na haijanakiliwa kutoka kwa kazi nyingine.
ii. Inaonyesha wazo, mtazamo au hisia binafsi za msanii.
iii. Haitakiwi kunakiliwa au kuigwa moja kwa moja kutoka kwenye kazi ya msanii mwingine.
iv. Wazo au mada iliyowasilishwa kwa namna mpya au isiyo ya kawaida.

### B.Ubunifu

i. Msanii anatakiwa kuonyesha fikra za kiubunifu katika matumizi ya rangi, upangaji wa picha, au mtindo.
ii. Kuwa na uvumbuzi katika jinsi mada ilivyofafanuliwa au kuonyeshwa.
iii. Msanii aweze kuchanganya vifaa, mbinu au mawazo yasiyo ya kawaida kuwasilisha ujumbe.
iv. Ubunifu unaonyeshe uwezo wa kwenda zaidi ya mambo ya kawaida na kuchunguza upekee wa sanaa.

Majaji wataangalia kazi zinazojitokeza kwa kuwa za kipekee, zenye mawazo mapya, na zenye ujumbe wa ndani sio tu kazi zenye ustadi, bali pia zinazogusa na kueleweka kiundani

### 2.Ufafanuzi wa mada

Katika mashindano ya sanaa ufafanuzi wa mada unahusu jinsi msanii anavyoelewa, kuelezea na kuwasilisha mada iliyotolewa kupitia kazi yake ya sanaa.

Mambo ya kuzingatia:

i. Uelewa: Msanii anaelewa vyema maana ya mada iliyotolewa.
ii. Uhusiano: Kazi ya sanaa ina uhusiano wa moja kwa moja na mada.
iii. Uwasilishaji: Ujumbe au simulizi inayohusiana na mada inaonyeshwa wazi kupitia rangi, maumbo, alama au mpangilio wa kazi.

**Ubunifu:** Msanii anatoa mtazamo wa kipekee au wa kibinafsi kuhusu mada, na sio kurudia tu mawazo ya kawaida.

**3.Ujuzi wa kitaalamu**

Katika mashindano ya sanaa ujuzi wa kitaalamu unahusu uwezo wa msanii kutumia vifaa, zana, na mbinu mbalimbali kwa ufanisi na ustadi katika kutengeneza kazi ya sanaa.

**Mambo muhimu ya kuzingatia**

i. Matumizi ya vifaa: Jinsi msanii anavyotumia rangi, penseli, brashi, udongo
ii. Udhibiti na usahihi: Usafi wa kazi, umakini wa maelezo na ufanisi wa kazi.
iii. Uelewa wa mbinu za kisanaa: Kama vile kivuli, kuchanganya rangi, mistari, umbile, uwiano na mtazamo.
iv. Uwasilishaji: Muonekano wa mwisho wa kazi ya sanaa iwe safi, imepangwa vizuri na kumaliziwa kwa umakini.
v. Vipengele na kanuni za uchoraji (Elements and Principles of Drawing).

**4. Mpangilio na mvuto wa kimaumbo**

Katika mashindano ya sanaa mpangilio na mvuto wa kimaumbo unazingatia jinsi vipengele vya sanaa vilivyopangwa na jinsi kazi ya sanaa inavyovutia machoni mwa mtazamaji.

**Mpangilio**

Huu ni mpangilio wa vipengele vya kuona kama vile mistari, maumbo, rangi, nafasi na umbile ndani ya kazi ya sanaa.

Mpangilio mzuri huongoza macho ya mtazamaji na huleta usawa, maelewano na umakini katika kazi.

**Mvuto wa kimaumbo**

Huu ni uzuri wa jumla na athari ya kihisia ya kazi ya sanaa.

Unahusisha ubunifu, upekee, maelewano ya rangi, mtindo na hali ya hisia inayotolewa na kazi.

**5.Athari ya kihisia au kitamaduni**

Hii inahusu jinsi kazi ya sanaa inagusa hisia au inaakisi maadili na utambulisho wa kitamaduni.

**Athari ya kihisia:**

i. Jinsi kazi ya sanaa inavyoamsha hisia kama furaha, huzuni, matumaini au tafakari.
ii. Inaonyesha uwezo wa msanii kuwasilisha hisia kupitia maonyesho ya kuona.

**Athari ya kitamaduni:**

i. Jinsi kazi ya sanaa inavyoonyesha vipengele vya kitamaduni, mila, imani au historia.
ii. Inaonyesha uhusiano wa msanii na utamaduni wake au jamii yake.

Kipengele hiki hupima jinsi kazi ya sanaa inavyogusa mtazamaji kihisia au kuhusiana na utambulisho wa kitamaduni na maana yake.

**KIAMBATISHO 02**

**MFANO WA FOMU YA MAJAJI KATIKA SHINDANO LA SANAA YA UCHORAJI**

| Na. | Kipengele Kikuu | Vigezo Vidogo / Maelezo | Alama | Alama za Jaji |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Uasili na ubunifu** | Upekee wa kazi ya sanaa, | | |
| | | Chimbuko na Uhalisia wa kazi | | |
| | | Fikra yakinifu na ubunifu mpya | | |
| | | matumizi ya nyenzo na vifaa katika (kwa) ubunifu | | |
| | | **Jumla ndogo** | | |
| 2 | **Uzingatiaji wa Mada** | Uhusiano wa kazi ya sanaa na mada husika | | |
| | | Namna ya uwasilishaji wa ujumbe | | |
| | | mtazamo wa kipekee wa kazi hiyo | | |
| | | **Jumla ndogo** | | |
| 3 | **Ujuzi wa Kitaalamu** | Matumizi Sahihi ya Vifaa vya Sanaa | | |
| | | Usafi, mpangilio na uzingatiaji wa maelekezo | | |
| | | Matumizi sahihi ya kivuli, uwiano, mtazamo na mlingano wa picha | | |
| | | **Jumla ndogo** | | |
| 4 | **Mpangilio na Mvuto wa Kimaumbo** | Mpangilio wa Vipengele | | |
| | | Mpangilio sahihi wa Rangi | | |
| | | Mvuto wa macho | | |
| | | **Jumla ndogo** | | |
| 5 | **Athari ya Kihisia au Kitamaduni** | Uwezo wa kugusa hisia za hadhira yake(kuwasilisha hisia furaha,huzuni,matumaini,tafakari | | |

SUPPORTED BY Vivo energy Tanzania